## MUHTASARI WA BODI YA ZABUNI KIKAO CHA ROBO YA KWANZA KILICHOFANYIKA TAREHE 01/11/2021

**MAHUDHURIO**

| JINA | WADHIFA |
|---|---|
| 1.HERMAN NJEJE | MWENYEKITI |
| 2.PAUL HUMBA | KATIBU |
| 3.GILBERT MBOWE | MJUMBE |
| 4.GLORIA KANG'OMA | MJUMBE |
| 5.MHEZIWA BUNDALA | MJUMBE |
| 6.CASMIR MSOFU | (MWANASHERIA ) MWALIKWA |

**WASIOHUDHURIA**

| | |
|---|---|
| 1.PASTORY M. MASHIKU | MJUMBE (KWA TAARIFA) |

**SEKRETARIETI**

| | |
|---|---|
| 1. JOSEPH MURWA | MWALIKWA |
| 2. SUZANA HAULE | MWALIKWA |

## AGENDA ZA KIKAO

1.Kufungua Kikao.

2.Kuridhia Agenda.

3.Kusoma na kuthibitsha Muhtasari wa kikao cha Bodi ya Zabuni cha tarehe 04/03/2021

4.Kupitisha Mpango wa Ununuzi wa mwaka 2021/2022.

5.Kupisha njia ya "Force Account" ili itumike katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa miradi ifuatayo:-

i) Ujenzi wa kituo cha Afya Ndola kiasi cha TZS 250,000,000.00

ii) Ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule za Sekondari Mbebe na Kafule kiasi cha TZS 37,500,000.00

iii) Ujenzi wa majosho na ukarabati wa kliniki za mifugo kiasi cha TZS 54,000,000.00

6.Kupitisha wazabuni watakaotumika kwa mwaka wa fedha 2021/2022

7.Kupitia na kujadili hoja za manunuzi zilizojitokeza katika ukaguzi wa mwaka wa fedha 2020/2021.

8.Kujadili na kupitisha Bajeti ya nyongeza kwa ajili ya miradi ya Ujenzi wa madarasa, nyumba ya Mtumishi, vyumba vya ICU na vyoo.

9.Kujadili na kupitisha ununuzi wa magari mawili na pikipiki moja ya Idara ya Afya.

10.Mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti

11.Kufunga kikao.

**AGENDA Na. HWI/TB/2021/2022/01 Kufungua Kikao**

Mwenyekiti alifungua kikao mnamo saa 10.50 asubuhi na kuwashukuru wajumbe kwa mahudhurio yao, Mwenyekiti aliwaomba wajumbe wawe huru kuchangia mawazo yao.

**AGENDA Na. HWI/TB/2021/2022/02 Kuridhia Agenda**

Katibu aliwasilisha agenda kumi na moja (11) kwenye kikao, Baada ya kuzipitia agenda hizo, wajumbe walizipokea na kuridhia ili zijadiliwe katika kikao hicho kama zilivyowasilishwa.

**AGENDA Na. HWI/TB/2021/2022/03 Kusoma na kuthibitsha Muhtasari wa kikao cha bodi ya zabuni cha tarehe 04/03/2021**

Muhtasari wa kikao cha tarehe 04/03/2021 ulisomwa mbele ya kikao hicho, kulikuwa na masahihisho madogomadogo ya kisarufi, Baada ya masahihisho hayo, wajumbe waridhia kuwa ni kumbukumbu sahihi za kikao hicho.

**AGENDA Na. HWI/TB/2021/2022/04 Kupitisha Mpango wa Ununuzi wa mwaka 2021/2022**

Katibu aliwasilisha mpango wa manunuzi wa mwaka wa fedha 2021/2022 katika kikao na wajumbe waliridhia na kupitisha mpango wa manunuzi huo ili uweze kutumika kama ilivyo kusudiwa katika mpango na bajeti ya Wilaya.

**AGENDA Na. HWI/TB/2021/2022/05 Kupitisha njia ya "Force account" ili itumike katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo**

Katibu aliwasilisha njia ya "Force Account" ili itumike katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Halmashauri kwa miradi ifuatayo:-

i) Ujenzi wa kituo cha Afya Ndola kiasi cha TZS 250,000,000.00
ii) Ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule za Sekondari Mbebe na Kafule kiasi cha TZS 37,500,000.00
iii) Ujenzi wa majosho na ukarabati wa kliniki za mifugo kiasi cha TZS 54,000,000.00

Aidha, ilielezwa kwamba, fedha hizo tayari zimekwisha pokelewa, hivyo, taratibu za ujenzi ziendelee.

Afisa Mifugo aliombwa kuwasilisha taarifa ya maeneo ambapo majosho hayo yatakapo jengwa , na mchanganuo wa kazi kwa kushirikisha idara ya ujenzi ili wapate michoro na Bill of quantities(BOQ) kulingana na mazingira halisi.

**AGENDA Na. HWI/TB/2021/2022/06 Kupitisha wazabuni watakaotumika kwa mwaka wa fedha 2021/2022**

Maelezo kuhusu orodha ya wazabuni ambao Halmashauri inatarajia kuwatumia kwa kipindi cha mwaka husika iliwasilishwa kwenye kikao. Ufafanunzi ulitolewa kuwa kuna baadhi ya wazabuni ambao tunalazimika kuwatumia kulingana na mazingira yetu kutokana na matumizi ya "Force account" kwenye miradi ya maendeleo. Kuna wazabuni ambao wamesajiriwa na GPSA na kuna wengine ambao hawajasajiriwa na GPSA lakini tunatarajia kufanya nao kazi.

Hivyo, kikao kiliridhia na kupitisha orodha ya wazabuni hao ili waweze kufanya kazi hizo, sharti ni kwamba wawe wanarisiti za kielektroniki za malipo (EFD Receipts) kwa kukiri mapokezi ya fedha wanazolipwa. Kwa upande wa Local fundi's waweze kukiri mapokezi ya fedha watakazolipwa kwa maandishi.

**AGENDA Na. HWI/TB/2021/2022/07 Kupitia na kujadili hoja za Manunuzi zilizojitokeza katika ukaguzi wa mwaka wa fedha 2020/2021**

Katibu aliwasilisha hoja za manunuzi zilizojitokeza katika ukaguzi wa mwaka wa fedha 2020/2021. Hoja hizo zilijadiliwa na kupatiwa majawabu. Aidha, kulikuwa na hoja iliyo husu punguzo la bei ya bati kutoka kiwanda cha bati ALAF ambacho kililipwa chote. Kikao kiliagiza kwamba Idara ya fedha ifuatilie malipo hayo ili kuona halmashauri ina faidika na punguzo la bei kwa bidhaa zinazonunuliwa toka kiwandani.

**AGENDA Na. HWI/TB/2021/2022/08 Kuridhia bajeti ya nyongeza kwa ajili ya miradi ya ujenzi wa Madarasa, Nyumba ya mtumishi, vyumba vya ICU na vyoo**.

Maombi ya kuomba bajeti ya nyongeza ipitishwe kwa ajili ya miradi ya ujenzi iliwasilishwa na Idara ya Mipango ili Bodi iridhie na kupitisha kwa mchanganuo ufuatao:-

i) Ujenzi wa madarasa shule ya msingi TZS 160,000,000.00
ii) Ujenzi wa masadarasa shule za sekondari TZS 620,000,000.00
iii) Nyumba ya mtumishi TZS 90,000,000.00
iv) Ujenzi wa Intensive Care Unit (ICU) TZS 250,000,000.00 .

**Jumla ni TZS 1,120,000,000.00**

Ufafanuzi ulitolewa kwamba, baada ya kupitishwa maombi hayo yatawasilishwa kwenye vikao vya kisheria vya Fedha ,Uongozi na Mipango (FUM) ili kuapata kibali cha kuweza kutekeleza.

Wajumbe waliridhia na kupitisha maombi hayo ya kiasi cha TZS **1,120,000,000.00**

Ili taratibu zingine ziendelee kwa muiibu wa sheria na miradi hiyo iweze kutekelezwa kwa wakati katika kipindi cha mwaka 2021/2022.

**AGENDA Na. HWI/TB/2021/2022/09 Kujadili na kupitisha ununuzi wa Magari mawili na pikipiki moja ya idara ya afya**

Maombi ya ununuzi wa magari mawili na pikipiki moja ya idara ya afya yaliwasilishwa kwenye kikao na kujadiliwa. Ilielezwa kwamba fedha za ununuzi wa vyombo hivyo imetengwa kwenye bajeti ya mwaka 2021/2022.

Hivyo, wajumbe waliridhia na kupitisha maombi hayo ili taratibu za kuomba vibali vya kununua uendelee kwenye Mamlaka husika kwa mujibu wa sheria na Miongozo ya Serikali.

**AGENDA Na.HWI/TB/2021/2022/10 Mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti**

Wajumbe walisisitiza kuwa, vikao vya Bodi ya Zabuni vifanyike kila Robo kwa mujibu wa sheria. Taratibu za malipo na posho za vikao izingatiwe kwa mujibu wa sheria. Hivi ni vikao vya kisheria kama vikao vingine. Hivyo, katibu afuatilie stahiki za wajumbe ili waweze kulipwa.

**AGENDA Na. HWI/TB/2021/2022/11 Kufunga kikao**

Mwenyekiti alifunga kikao mnamo saa 14.20 mchana kwa kuwashukuru wajumbe kwa michango yao ya mawazo na uvumilivu walio uonesha hadi kufanikisha kikao hicho.

Umethibitishwa na

**KATIBU**

15/1/2022.
**TAREHE**

**MWENYEKITI**